

yaboresha huduma tuo cha Afya Chanika

utoaji wa huduma ya afya," alisema.

Alisema utekelezaji wa mradi umehusisha ulazaji wa mabomba makubwa ya inchi nne, tatu na mbili kwa umbali wa kilometra 1,550 kwenda kituoni hapo.

"Mradi tunautekeleza kwa kutumia chanzo cha maji cha tenki la Kisarawe lenye ujazo wa litu milioni sita, litakosambaza maji kwa msukumo mkubwa kwenda Kituo cha Afya Chanika," alisema.

Pia, alieleza kaya 200 za mitaa ya Nyeburu, Nguvu mpya na barabara ya Kilimahewa zinazopitwa na mradi huo zitanufaika.

"Mpaka hivi sasa tumetekeliza mradi kwa asilimia 85, ambapo mwisho wa mwezi huu wa Juni huduma katika Kituo cha Afya Chanika itaanza kupatikana," alisema.

Naye, Mganga Mfawidhi wa Kituo cha Afya Chanika, Pascal Nkii, alisema ukosefu wa huduma ya maji

umesababisha matumizi makubwa ya fedha kwa watu binafsi na unaathiri uendeshaji wa mitambo ya afya, hivyo kulazimika kutumia gharama kubwa ya kununu maji ya mitaani, ambayo wakati mwininge yanakuwa na chumvi.

Alibainisha kwa wastani kituo hupokea wagonjwa 750 kwa siku, hivyo hupata changamoto hususan wakati wa kuhudumia wagonjwa, bila maji safi na kuongeza mradi utakuwa mkombozi mkubwa kwao.

Mkazi wa Chanika, Mwajuma Shomari aliyejhudumiwa kituoni hapo, aliipongeza DAWASA kwa kuondoa changamoto ya ukosefu wa maji kwa kuwa wanatumia maji ya chumvi kwa muda mrefu ambayo siyo salama kiafya.

Alisisitiza huduma ya maji safi katika kituo cha afya ni muhimu hususan kwa huduma ya mama na mtoto na itawasaidia wanawake na watoto wakati wakipata huduma.

Kamati ya ufundi ya serikali mtandao yakutana Dodoma

NA MWANDISHI WETU

KAMATI ya Ufundu ya Serikali Mtandao, imekutana kwa mara kwanza jijini Dodoma, kujadili mambo mbalimbali ikiwemo namna ya utekelezaji wa majukumu yake, kuhakikisha jitihada za serikali mtandao zinamarika na kuleta tija kwa umma.

Kikao hicho kilifanyika jijini hapa, juzi katika Ofisi za Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-G) na kuongozwa na Kairu Mwenyekiti Eric Kitali ambaye pia ni Mkurugenzi wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI).

Akizungumza katika kikao hicho, Eric alisema kamati ipo kwa mujibu wa kifungu namba 17 cha sheria ya Serikali Mtandao ya mwaka 2019, ambapo miiongoni mwa majukumu yake ni kutoa ushauri wa kitaalamu, kuhakikisha utekelezaji wa serikali mtandao unakuwa ni wenye tija na kuongeza ufanisi wa utendaji kazi na utoaji wa huduma kwa umma.

Mkurugenzi huyo alieleza kamati ina wajumbe wachache ikililinganishwa na idadi ya wizara na taasisi za serikali zilizopo, hivyo aliwasili wajumbe kutenda haki kwa kuwajibika na kuhakikisha wanatoa ushauri wenye tija eneo la TEHAMA kuhakikisha serikali mtandao inaimarika na kuleta tija kwa serikali.

"Ikiwa kamati hii itafanikiwa kufanya mifumo ya TEHAMA katika taasisi za umma izungumze tutakuwa tumeaisida sana serikali, kwa kuwa itaokoa rasilimali fedha na rasilimali watu," alisisitiza.

Katibu wa kamati hiyo, Sylvani Shayo ambaye pia ni Mkurugenzi wa Udhibili na Usalama wa TEHAMA e-G, aliyataja baadhi ya majukumu ya kamati kwa mujibu wa kifungu Na 17 (4) cha Sheria ya Serikali Mtandao ya mwaka 2019 ni kupitia na kutoa mapendekezo kuhusu Sera ya Serikali Mtandao itakayotekelezwa katika taasisi za umma, kupitia na kutoa mapendekezo kuhusu mpango mkuu wa serikali mtandao na mkaatiki wake utakaotekeliza na taasisi zote za umma.

Majukumu mengine ni kupitia na kutoa mapendekezo ya miradi na programu za kitaifa za serikali mtandao na kutoa miongozo ya kiufundi kutatua migogoro katika utekelezaji wa miradi mikubwa ya TEHAMA kwa taasisi za umma.

Pia, kuishauri kamati ya kitaifa ya serikali mtandao kuhusu masuala ya serikali mtandao, kuanda ripoti za robo mwaka na kuziwasilisha katika kamati hiyo na kutekeleza majukumu mbalimbali yatakayotolewa na Mamlaka ya Serikali Mtandao na Kamati ya kitaifa ya Serikali Mtandao.

Alisema kamati iliazimia kuweka mikakati ya kupunguza uruduwa wa mifumo na kuhakikisha mifumo yote ya TEHAMA, katika taasisi za umma inawasiliana na kubadilishana taarifa kupitia Mfumo Mkuu wa ubadilishanaji taarifa serikalin (GoVESB).

Katika hatua nyingine, kamati ilimchagua Mkurugenzi wa TEHAMA Mamlaka ya Vitambulisho yya Taifa (NIDA), Connie Francis, kuwa Makamu Mwenyekiti wa kamati hiyo.

Wajumbe wa kamati ni wakuu wa TEHAMA kutoka wizara na taasisi mbalimbali za serikali wakiongozwa na Mwenyekiti Priscus Kiwango kutoka Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na Katibu Shayo

na Usafi
Salaam
atekeleza
maji safi
kilichopo

muhimu
rahisisha
vananchi
iicho.

Mhandisi
a hayo
mradi
uwaitikanaji
ambacho
imekuwa

za mradi
io cha ya
vengi wa
atambua
nu katika



Rosemary Senyamule (katikati), akikagua ujenzi wa Uwanja wa Mashujaa, aajengwa katika Mji wa Serikali Jiji Dodoma, jana.

ata bidhaa marufuku

za ndani zilizopigwa marufuku, ambazo zinagusana na ngozi na huko zilikotoka zimeshavaliwa, hivyo hajulikani mtumiaji alikuwa na magonjwa gani.

"Hizi nguo za ndani za mitumba zinaweza kuleta magonjwa ya ngozi, tulishatoa elimu kwa wauzaji na waingizaji wa nguo za mitumba, kwamba nguo za ndani hazitakiwi kutumika nchini," alisema.

Alifafanua hivi sasa wameamua kushuka na kwenda kutoa elimu kwa wananchi kuhusu madhara ya nguo za ndani za mitumba na kuziondoa sokoni.

Hata hivyo, alieleza changamoto ni wafanyabiashara wasio waaminifu wanaozipitisha katika njia za panya, kwa kuwa wangezipitisha njia halali

3, Alananga alisema yalisapigwa marufuku kutumika nchini kutokana na kutokidhi viwango kwa kuwa yanapotumika magari yanaweza kusababisha moto au breki kufeli na kusababisha uharibifu wa mali na hata vifo.

Kwa upandewa nyaya za umerme, Alananga alisema zilizokamatwa zilishakatazwa kuingizwa sokoni, kwa sababu zinaweza kuunguza vitu zikiwemo nyumbu.

Aliongeza katika operesheni hiyo walikagua waduu 651 na watu 154 ambapo waliokutwa na makosa ya kuza bidhaa hizo wamepewa siku 14

za kueleza ni wapi walizinunua na baada ya hapo watafikishwa mahakamani kwa mujibu wa sheria na watatakiwa kulipia gharama za kuziteketeza.

Ukaguzi

ELIMU

Alifafanua hivi sasa wameamua kushuka na kwenda kutoa elimu kwa wananchi kuhusu madhara